THE REPUBLIC OF UGANDA
Ministry of Education and Sports

# ADVANCED SECONDARY CURRICULUM




# KISWAHILI ASSESSMENT GUIDELINES

NCDC
NATIONAL CURRICULUM DEVELOPMENT CENTRE

2026

# ADVANCED SECONDARY
CURRICULUM

# KISWAHILI
# ASSESSMENT GUIDELINES

2026

NCDC
NATIONAL CURRICULUM
DEVELOPMENT CENTRE

Copyright © National Curriculum Development Centre, Uganda 2026

A product of the National Curriculum Development Centre for the Ministry of Education and Sports with support from the Government of Uganda

National Curriculum Development Centre
P.O. Box 7002,
Kampala- Uganda
www.ncdc.co.ug

**ISBN:** 978-9970-494-61-3

All rights reserved: No part of this publication may be reproduced, stored in a retrieval system or transmitted in any form or by any means, electronic, mechanical, photocopying, recording, or otherwise, without the prior permission of the copyright holder

# Content

**Acknowledgements** ........ v

**1. Utangulizi** ........ 1

1.1 Malengo Ya Tathmini ........ 1

1.2 Uhusiano Kati Ya Malengo Ya Tathmini, Vipengele Vinavyohusiana Vya Ujenzi Wa Uwezo, Na Silabasi ........ 2

**2. Jedwali La Vipengele Vinavyohusiana Vya Ujenzi Wa Uwezo (Table Of Constructs)** ........ 4

**3. Muundo Wa Karatasi Za Tathmini** ........ 12

**4. Maelezo Ya Viwango Vya Utendaji.** ........ 32

## Acknowledgements

The National Curriculum Development Centre (NCDC) is indebted to the Government of Uganda for financing the development of these Assessment Guidelines to support the implementation of the Advanced Secondary Curriculum.

Our gratitude goes to the Ministry of Education and Sports for overseeing the development process, the Curriculum Task Force of the Ministry of Education and Sports for the guidance and timely decisions whenever necessary, and members of the public who made helpful contributions towards shaping these Guidelines.

NCDC is also grateful to UNEB, Members of Parliament, schools, universities, and other tertiary institutions, the writing panels, critical reviewers, and professional bodies for their contribution towards the design and development of these Assessment Guidelines. To all those who worked behind the scenes to finalise the production of these Guidelines, your efforts are invaluable.

NCDC takes responsibility for any shortcomings that might be identified in this publication and welcomes suggestions for effectively addressing the inadequacies. Such comments and suggestions may be communicated to NCDC through P. O Box 7002, Kampala, or Email: admin@ncdc.go.ug or on the Website: www.ncdc.go.ug

Dr Bernadette Nambi Karuhanga
**Director**
**National Curriculum Development Centre**

# KISWAHILI

# 1. Utangulizi

Tathmini ya Mwisho ya Fasihi ya Kiswahili itatekelezwa na Bodi ya Mitihani ya Taifa la Uganda (UNEB). Tathmini hii ya somo la Kiswahili itaongozwa na malengo mawili ya tathmini yanayotokana na vipengele viwili vya ujenzi wa uwezo (constructs). Maswali ya tathmini yataandaliwa kwa kuzingatia kiwango cha mkusanyiko wa vipengele vinavyohusiana vya ujenzi wa uwezo, ili kuwawezesha wanafunzi kutumia kwa pamoja maarifa, stadi na maadili yanayotokana na mada mbalimbali ndani ya kila kipengele husika, kwa lengo la kushughulikia changamoto au tatizo la kijamii.

## 1.1 Malengo Ya Tathmini

Malengo ya tathmini ya Fasihi ya Kiswahili yanazingatia uwezo wa mwanafunzi katika:

**Lengo 1:** Kuchambua kazi za kifasihi kwa kuzingatia vipengele kama maudhui, wahusika, mtindo, ploti na vingine.

**Lengo 2:** Kutunga kazi asilia za kifasihi kwa kutumia mbinu za kisanaa zinazofaa.

## 1.2 UHUSIANO KATI YA MALENGO YA TATHMINI, VIPENGELE VINAVYOHUSIANA VYA UJENZI WA UWEZO, NA SILABASI

Jedwali lifuatalo linaonesha uhusiano kati ya malengo ya tathmini, vipengele vya ujenzi wa uwezo vinavyohusiana, na mada zinazochangia kila kipengele.

**Jedwali 1:**

*Jedwali linaloonesha uhusiano kati ya malengo ya tathmini, vipengele vya ujenzi wa uwezo vinavyohusiana na mada zilizomo kwenye mtaala.*

| Malengo Ya Tathmini | Vipengele Vinavyohusiana Vya Ujenzi Wa Uwezo (Construct) | Ufafanuzi Wa Vipengele Vinavyohusiana Vya Ujenzi Wa Uwezo | Mada Katika Silabasi |
|---|---|---|---|
| **Lengo 1:** Kuchambua kazi za kifasihi kwa kuzingatia vipengele kama maudhui, wahusika, mtindo, ploti na vingine. | Uchambuzi na uhakiki wa kazi za fasihi | Kuchambua na kuhakiki kazi mbalimbali za nathari, mashairi, tamthilia na riwaya kwa kuzingatia vipengele vya kifasihi ili kuimarisha ustadi wa kuandika, | 1) Nathari<br>2) Ushairi<br>3) Tamthilia<br>4) Riwaya |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | mawasiliano bora, kuelimisha, kuburudisha, kuendeleza na kukuza maadili, pamoja na kujikimu kiuchumi. | |
| **Lengo 2:** Kutunga kazi asilia za fasihi kwa kutumia mbinu za kisanaa ili kufikisha mawazo kwa ufasaha na staha katika mazingira ya kijamii na kielimu. | Uandishi bunifu wa kazi za fasihi | Kutunga, kuchapisha na kuandaa kazi bunifu za fasihi kama hadithi fupi, ushairi, nathari, tamthilia na riwaya kwa kuzingatia vipengele vya kifasihi, ili kuburudisha, kukuza maadili, kuimarisha mawasiliano, kujipatia kipato na kuendeleza ustadi wa uandishi bora. | 1) Nathari<br>2) Ushairi<br>3) Tamthilia<br>4) Riwaya |

## 2. JEDWALI LA VIPENGELE VINAVYOHUSIANA VYA UJENZI WA UWEZO (Table of Constructs)

Jedwali lifuatalo linafafanua vipengele vya ujenzi wa uwezo wa mwanafunzi vinavyofanana katika somo la Kiswahili, yaani umilisi / matokeo ya ujifunzaji yanayounda kipengele husika, uwezo unaotarajiwa kwa mjifunzaji, pamoja na mambo ambayo mtathmini anapima katika kazi ya mwanafunzi kama ushahidi wa kufanikisha matokeo yaliyokusudiwa ya ujifunzaji (viashiria vya ustadi).

| **Vipengele Vinavyohusiana vya Ujenzi wa Uwezo (Construct)** | **Matarajio ya Ujifunzaji** *Mwanafunzi aweze;* | **Uwezo wa** | **Viashiria vya Ustadi** | **Kiwango cha Ugumu** |
|---|---|---|---|---|
| 1) **Uchambuzi na uhakiki wa kazi za fasihi**<br><br>Kuchambua na kuhakiki kazi mbalimbali za nathari, | a) Kueleza maana na sifa za ushairi, tamthilia, riwaya na nathari katika matini teule.<br>b) Kubainisha aina mbalimbali za tamthilia na riwaya | i) Kuchanganua kazi mbalimbali za fasihi.<br>ii) Kubainisha aina mbalimbali za tanzu za fasihi.<br>iii) Kutathmini na kupambanua vipengele vya muundo vya kazi | 1) Alipambanua aina mbalimbali za nathari<br>2) Alifanya utafiti kuhusu fasihi simulizi, fasihi andishi na sifa zake<br>3) Alipambanua vipengele vya fasihi<br>4) Alisimulia hadithi mbalimbali za Kiswahili | Juu<br><br>Juu |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| mashairi, tamthilia na riwaya kwa kuzingatia vipengele vya kifasihi ili kuimarisha ustadi wa kuandika, mawasiliano bora, kuelimisha, kuburudisha, kuendeleza na kukuza maadili, pamoja na kujikimu kiuchumi. | na kudhihirisha tofauti zake.<br>c) Kuchambua matumizi ya lugha na mbinu za kisanii (kama tamathali za usemi, taswira, sitiara, tashibihi, tashihisi) katika ushairi, tamthilia, riwaya na kazi za nathari, kwa kuangazia jinsi zinavyoibua na kukuza ujumbe wa matini.<br>d) Kutathmini vipengele vya mtindo na mitazamo mbalimbali katika | mbalimbali za fasihi, ikiwemo riwaya, tamthilia, nathari na ushairi.<br>iv) Kuchambua mashairi ya Kiswahili, vina, bahari, vipande, na urefu wa mishororo.<br>v) Fafanua ujumbe na umuhimu wa ushairi katika jamii.<br>vi) Kukariri na kusikiliza mashairi yaliyorekodiwa na kuyakumbuka.<br>vii) Jadili dhima ya vipengele vya muundo katika ukuzaji wa ushairi. | 5) Aliwasilsha kazi bunilizi<br>6) Alichambua aina mbali mbali za mashairi<br>7) Alikariri mashairi katika Kiswahili<br>8) Alitunga mashairi katika Kiswahili<br>9) Alichambua tamthilia za Kiswahili<br>10) Alibuni michezo mifupi mifupi ya kuigiza<br>11) Aliigiza michezo katika majukwaa tofauti tofauti<br>12) Alichambua aina mbalimbali za riwaya<br>13) Alifautisha riwaya na tanzu nyingine za fasihi<br>14) Alipambanua tamathali za usemi namna zinavyoweza | Wastani<br><br>Juu<br><br>Juu |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | kazi za nathari, na kueleza jinsi vinavyosaidia kujenga upekee wa kisanii na uelewa wa msomaji kuhusu hadithi.<br>e) Kuchambua hali, hisia na toni katika mashairi na kuelewa jinsi vinavyoibua ujumbe.<br>f) Kudhihirisha uelewa wa muundo wa shairi kwa kuzingatia mada, beti, vipande na mizani, pamoja na kupambanua na kuchanganua | viii) Fafanua na kupambanua mbinu za lugha, tamathali za usemi na mtindo katika riwaya, tamthilia, nathari na ushairi.<br>ix) Kufafanua mbinu za usimulizi katika riwaya na kueleza umuhimu wake katika kufanikisha ujumbe wa mwandishi.<br>x) Fanya utafiti kuhusu dhana na sifa za riwaya, pamoja na vipengele vya wahusika, mandhari, ploti na migogoro.<br>xi) Kuelezea mchango wa mandhari katika | kutumika katika kusawiri ujumbe wa mwandishi wa riwaya<br>15) Alichanganua mbinu mbali mbali za lugha katika matini husika<br>16) Alipambanua mitindo mbalimbali kutoka katika matini za kifasihi<br>17) Alisimulia kiufasaha matini za kinathari<br>18) Alieleza umuhimu wa vipengele vya muundo katika kukuza ujumbe katika mashairi<br>19) Alikariri mashairi ya Kiswahili<br>20) Alielezea ujumbe unaopatikana kutokana na mashairi | Wastani<br><br>Juu<br><br>Wastani |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | bahari za ushairi kwa vigezo vya vina, urefu wa mishororo na mpangilio wa vipande.<br>g) Kuchambua vipengele vya tamthilia kama wahusika, mandhari, ploti, mbinu za uigizaji na maelekezo ya jukwaa.<br>h) Kueleza mbinu za usimulizi na mbinu mbalimbali za uandishi katika riwaya na kazi za nathari (kama mazungumzo, | ujenzi wa wahusika na ujumbe wa mwandishi.<br>xii) Kusoma matini teule za riwaya kwa Kiswahili sanifu na kuchambua maudhui na dhamira zinazojitokeza.<br>xiii) Kulinganisha madondoo ya mtazamo tofauti kwa kurejelea dhima na athari zake.<br>xiv) Pambanua mbinu za uigizaji wa tamthilia na kufafanua umuhimu wa maleba katika sanaa ya maigizo. | 21) Alichambua vipengele vya wahusika, mandhari na ploti.<br>22) Alifafanua mbinu za usimulizi katika riwaya<br>23) Alileza umuhimu wa usimulizi katika kufanikisha ujumbe wa mwandishii<br>24) Alichambua maudhui kutoka kwa kazi za fasihi.<br>25) Alipambanua dhamira ya waandishi tofauti wa nathari<br>26) Alipambanua sehemu ya muundo wa ushairi<br>27) Alieza bahari za ushairi. | Juu<br>Wastani<br>Wastani |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | maelezo na mtazamo).<br>i) Kuchambua maudhui na dhamira katika riwaya na tamthilia teule na kueleza athari yake kwa msomaji.<br>j) Kufafanua na kujadili dhana ya mgogoro katika riwaya na tamthilia, na umuhimu wake katika uendelezaji wa hadithi.<br>k) Kudhihirisha uelewa wa ujumbe katika mashairi ya kimapokeo na huru. | xv) Fanya utafiti kuhusu matumizi ya maleba katika tamthilia.<br>xvi) Fanya utafiti kuhusu aina mbalimbali za mashairi ya Kiswahili na kuainisha kwa kurejelea vigezo husika. | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2) **Utunzi bunifu wa kazi za fasihi**<br><br>Kutunga, kuchapisha na kuandaa kazi bunifu za fasihi kama hadithi fupi, ushairi, nathari, tamthilia na riwaya kwa kuzingatia vipengele vya kifasihi, ili kuburudisha, kukuza maadili, kuimarisha mawasiliano, kujipatia kipato | a) Kuunda na kusimulia kazi asilia za nathari, kutumia mbinu mbalimbali za usimulizi na vipengele vya kisanii ili kuwasilisha kwa ufanisi maudhui, kujenga wahusika na kumvutia msomaji. (s, v, a, gs)<br>b) Kutunga aina mbalimbali za mashairi asilia kwa kutumia mbinu anuwai za kishairi kudhihirisha ubunifu na uelewa wa miundo ya kishairi. (u, s, a) | i) Buni maigizo mafupi na kuyaigiza darasani na katika majukwaa tofauti.<br>ii) Tengeneza maleba ambayo yanaweza kutumika katika maigizo.<br>iii) Igiza michezo na tamthilia za Kiswahili ulizopewa.<br>iv) Kusimulia kazi za nathari<br>v) Kutunga kazi za nathari<br>vi) Kudhihirisha namna ya kuibuka na mada ya utunzi wa ushairi<br>vii) Kudhihisha matumizi ya vipengele vya uhuru wa mshairi katika kutunga mashairi. | 1) Alifanya mpango kazi wa mradi wa uandishi<br>2) Alitunga kazi ya nathari<br>3) Alidhihirisha matumizi ya vipengele vya Uhuru wa Mshairi katika utunzi wa mashairi<br>4) Alipambanua maelekezo ya jukwaa katika tamthilia kuendeleza maonesho na matendo katika tamthilisha<br>5) Aliandaa mpango kazi wa sura za riwaya<br>6) Aliandika riwaya kamili<br>7) Aliandika upya kazi za nathari kwa kutumia tamathali za usemi | Juu<br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br>Juu |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| na kuendeleza ustadi wa uandishi bora. | c) Kuandika sura za riwaya ili kudhihirisha uelewa wa mbinu za usimulizi, ujenzi wa wahusika na maudhui. (u, gs, v, a)<br>d) Kutunga na kuigiza maonyesho ya tamthilia kwa kuzingatia muundo sahihi. (k, u, v, a, gs) | viii) Kudhihirisha utunzi wa maelekezo ya jukwaa katika tamthilia<br>ix) Fanya mpango kazi wa sura za riwaya<br>x) Andika muhtasari wa sura za riwaya<br>xi) Tunga kazi ya riwaya kwa kurejelea mpango kazi ulioandaa<br>xii) Andika upya matini husika ulizopewa kutumia thamathai za usemi<br>xiii) Andika kazi ya nathari kwa kuhusisha tamathali za usemi<br>xiv) Andika shairi kwa kurejelea mtazamo wa mtu mashuhuri | 8) Alitunga mashairi yanayodhihirisha hali, hisia na toni<br>9) Alifafanua vigezo muhimu vinavyozingatiwa wakati wa utunzi wa tamthilia<br>10) Alitunga tamthilia fupi katika Kiswahili<br>11) Aliigiza tamthilia teule katika Kiswahili<br>12) Alikariri mashairi<br>13) Alitunga mashairi<br>14) Alibuni hadithi fupi | Juu<br><br>Juu |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | xv) Tunga onyesho ama sehemu moja ya tamthilia<br>xvi) Igiza maonesho kutoka tamthilia<br>xvii) Sikiliza na kukariri mashairi yaliyorikodiwa | | |

# 3. Muundo Wa Karatasi Za Tathmini

Fasihi ya Kiswahili ya Sekondari ya Juu ina karatasi za utathmini mbili. Hii inalenga kuhakikisha vipengele vyote vya mtaala vimezingatiwa kikamilifu. Karatasi ya Kwanza hupima uwezo wa mwanafunzi katika Uchanganuzi wa Fasihi, ilhali Karatasi ya Pili humpima mwanafunzi katika Utunzi wa Kazi za Fasihi. Karatasi ya kwanza itakuwa na sehemu mbili ilhali karatasi ya pili itakuwa na sehemu moja tu. Sehemu hizi zote zitakuwa na maswali yanayokidhi malengo ya tathmini.

**KARATASI YA KWANZA**

Karatasi ya kwanza ina Sehemu A na B. Sehemu A itakuwa na matini itakayowahitaji wanafunzi kujibu maswali.

Sehemu B itakuwa ya maswali ya kuchanganua vitabu teule. Yatakuwa maswali ya insha. Sehemu hii itakuwa na maswali matatu. Mwanafunzi atachagua maswali mawili kutoka sehemu hii. Maswali hayo yote mawili yatafanikisha lengo la kwanza. Mwanafunzi ataonesha ujuzi wake wa kuchambua kazi za fasihi kutokana na tanzu za fasihi ambazo amesoma darasani. Karatasi hii ya Kwanza itachukua saa tatu ambapo ni dakika 180.

**KARATASI YA PILI**

Karatasi hii inamtathmini mwanafunzi katika utunzi bunifu wa kazi za kifasihi. Itakuwa na maswali mawili. Mwanafunzi atachagua swali moja.

Swali hili ambalo ni la utunzi litafanikisha lengo la pili ambapo mwanafunzi anaonesha ujuzi wake wa kutunga kazi za kifasihi kutoka katika tanzu zote za fasihi ambazo amesoma kwa miaka yake miwili. Karatasi ya Pili itachukua saa tatu ambapo ni dakika 180. Jumla ya muda kwa karatasi zote mbili ni dakika 360.

**MIFANO YA KARATASI ZA TATHMINI**
**KARATASI YA KWANZA: UCHANGANUZI WA FASIHI**

**KISWAHILI**

**Karatasi ya Kwanza**

Novemba, 2025

**Muda:** Saa 3

**UGANDA ADVANCED CERTIFICATE OF EDUCATION**

**SAMPLE EXAMINATION PAPER**

**KISWAHILI**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA:**
**Karatasi hii ina sehemu mbili; A na B**
Sehemu ya A ina swali moja la lazima
Sehemu ya B ina maswali matatu ya insha kutokana na vitabu vilivyoteuliwa. Unapaswa kujibu maswali mawili katika sehemu hii.

**SEHEMU A**

1) **Soma kisa kifuatacho kisha jibu swali lililo chini:**

**Manufaa na Changamoto za Simu**
Simu ya mkononi inaweza kuwa rafiki wa maarifa na adui wa mafanikio. Ilianza kama zawadi kwa Amina, mwanafunzi wa kidato cha tano, alipofaulu mtihani wa mwisho wa muhula wa pili. "Huu ni ufunguo wa dunia," baba yake alisema akimpa simu yenye mwangaza wa kutisha.

Amina alitumia simu hiyo kujiunga na vikundi vya *WhatsApp* vya masomo, kuangalia video za kihistoria kwenye *YouTube,* na hata kuhifadhi notisi kwenye *Google Drive.* Alijifunza mbinu mpya za kuandika insha kupitia vikundi mbalimbali. Simu ikawa ni mwalimu wake wa pili na darasa linalotembea.

Lakini… polepole, nyota ya matumaini ikaanza kufifia. Mitandao ya kijamii ilimvutia kama asali kwa nyuki, na muda wake wa kujifunza ukaanza kuliwa na video za kuchekesha kwenye *tiktok,* na *instagram.* Kulikuwa pia muziki wenye maudhui ya watu wazima na picha zisizo na maadili zisizofaa kutazamwa na wototo walio chini ya miaka kumi na nane. Alianza kupoteza mwelekeo, akasahau vitabu na kuikumbatia simu kama mlezi anavyomkumbatia mtoto wake. Ulevi wa kidijitali ukamteka kupindukia, usiku mzima angeumaliza akiwa kwenye simu na usingizi kwake ukawa mgeni. Darasani alisahaulika miongoni mwa wanafunzi wazuri.

Simu ile ile ya matumaini ikageuka kuwa upanga wenye makali pande zote. Alipoanguka mtihani wake wa mwisho wa muhula wa tatu, alilia. “Simu yangu imeniharibu!” Alilia kwi kwi kwi!

“Simu ilinikosesha usingizi. Simu ilinifanya nisahau vitabu. Lakini mama yake alimwambia, “Mtoto wangu, simu ndiyo ya kulaumiwa? Simu siyo mbaya, ni chaguo lako. Umejiangamiza mwenyewe.”

**Swali:** Kwa kurejelea kisa hiki, changanua mbinu za sanaa zilizotumika na jinsi zinavyosaidia kuwasilisha ujumbe.

**SEHEMU B**

2) **Soma kisa hiki kisha jibu swali:**

Katika kazi nyingi za fasihi, waandishi wamekuwa wakionesha mateso yanayowapata wanawake kutokana na mila na desturi za kijamii. Mara nyingi wanawake huonekana wakinyimwa elimu, wakidhulumiwa kimwili na kiakili, au wakinyimwa fursa za maendeleo. Wengine hukumbana na unyanyasaji na dhuluma za kijamii zinazowanyima haki ya kujieleza na kujiendeleza.

**Swali:** Kwa kurejelea mifano kutoka katika kitabu chochote cha fasihi ulichosoma, Jadili jinsi haki za wahusika wa kike zinavyoweza kulindwa na kuendelezwa.

3) **Soma kisa hiki kisha jibu swali:**

Waandishi wa kazi za fasihi wamekuwa mstari wa mbele kuonesha hali za ukandamizaji wa wanyonge kupitia hadithi, mashairi na tamthilia, wakihimiza jamii kupinga uonevu na kutetea haki za binadamu. Jamii nyingi bado zinakabiliwa na changamoto kama watu kufanya kazi kwa malipo duni, kupokonywa mali, watoto kunyimwa haki ya elimu, na hali nyingine za ukandamizaji. Hali hizi husababisha ukosefu wa amani na kuzoroteka kwa maendeleo ya jamii.

**Swali:** Kwa kurejelea kazi yoyote ya fasihi ambayo umesoma darasani, changanua jinsi unavyoweza kuhamasisha jamii kukomesha ukandamizaji wa wanyonge kama unavyodhihirishwa.

4) **Soma kisa kisha jibu maswali:**

Shule ya Sekondari ya Pagirinya iliandaa mashindano ya utunzi wa mashairi kwa wanafunzi wa kidato cha tano, yakiwa na mada: Mabadiliko ya Hali ya Anga. Pendo, mmoja wa washiriki, aliandika shairi lililoshinda nafasi ya kwanza. Hata hivyo, baadhi ya washiriki walinung'unika kwamba shairi hilo lilitumia maneno yaliyokiuka kanuni za sarufi kwa makusudi. Kwa mtazamo wao, mashairi yao ndiyo yaliyostahili kushinda kwa kuwa yaliandikwa kwa kuzingatia sarufi kikamilifu. Mfano wa shairi la Pendo:

**Hali ya Anga**

Yetu anga ni angavu, ina hewa ilo nzuri,
Mbingu hubakia kavu, mwezi hasa Januari,
Maji huwa toshelevu, kiangazi cha hatari.

Mawingu mavundevunde, na mepesi hutokea,
Hutaka watu wapande, masika kiongelea,
Kunyesha kila upande, kote ikaloweshea.

Muvua za rasharasha, mara nyingi haziishi,
Zinakoma zikinyesha, kuvuna haijulishi,
Yabidi kujiendesha, shughuli zako kijeshi

Kipupwe huwa baridi, upepo watetemesha,
Kwa masweta inabidi, kila mtu kujivisha,
Kutetemeka kizidi, ugonjwa kukuangusha.

Mvua fupi za vuli, mara nyingi septemba,
Huu msimu wa pili, watapanda hata pamba,
Wakatumia akili, wakayalima mashamba.

Ya anga nimeshasema, ni kuzuri sana kwetu,
Huanza mchana mwema, na usiku poa petu,
Twaliona jua wima, tushukuru kila kitu.

**Swali:** Kwa kurejelea shairi hili, dhihirisha namna Pendo alivyokiuka kanuni za kisarufi katika utunzi wake.

**MWISHO**

**KARATASI YA PILI: UTUNZI WA KAZI ZA FASIHI**

**KISWAHILI**

**Karatasi ya 2**

Novemba, 2025

**Muda:** Saa 3

**UGANDA ADVANCED CERTIFICATE OF EDUCATION**

**SAMPLE EXAMINATION PAPER**

**KISWAHILI**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA:**
**Karatasi hii ina maswali mawili. Unastahili kujibu swali moja tu.**
Unapaswa kutunga kazi ya fasihi kwa kurejelea kisa ulichopewa.

**AMA**

1) **Soma kisa na ujibu swali:**
Uhusiano wa kimapenzi kati ya wavulana na wasichana umeanza kuenea sana, hususan miongoni mwa wanafunzi. Hali hii imesababisha changamoto nyingi na kushuka kwa maadili ya vijana katika shule za sekondari. Licha ya walimu kutoa maonyo na nasaha, wanafunzi wengi wanayapuuza, jambo linalosababisha baadhi ya wasichana kupata mimba wakiwa bado wadogo, huku baadhi ya wavulana wakijikuta na matatizo mengine mkiwemo kufungwa gerezani. Tukio hili limezua mjadala mpana kuhusu mimba za mapema. Jamii pia imejiuliza maswali kadhaa kuhusu nafasi ya wazazi, walimu, na jamii kwa ujumla katika kulea na kulinda maadili ya kizazi cha sasa. Wilaya yako imetoa fursa kwa wanafunzi wa Kiswahili kushiriki katika uandishi bunifu kuhusu suala hili.

**Swali:** Kwa kuzingatia vipengele vya utunzi wa kazi ya fasihi, tunga kitendo kimoja cha tamthilia kwa kutumia maneno kati ya 1500 - 2000 ukidhihirisha suluhisho la suala hili.

**AU**

2) **Soma kisa na ujibu swali:**
**Kisa**
Katika kijiji cha Kijani Bora, wakazi wamekuwa wakikabiliwa na changamoto kubwa ya uchafuzi wa mazingira. Watu wametelekeza maadili ya utunzaji wa mazingira kwa kutupa taka ovyo, kulima kwenye vinamasi, kukata miti ovyo, kukata na kuchoma miti kwa ajili ya mikaa.
Mito imeanza kukauka, hewa imekuwa chafu, na wanyama wamekosa makazi. Shule ya sekondari ya kijijini humo imeamua kuandaa shindano la ushairi wa kitarbia, ili kuwahamasisha wanafunzi kutumia sanaa ya lugha kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kulinda mazingira.
**Swali**
Kwa kuzingatia vipengele vya utunzi wa shairi la kitarbia, tunga shairi lililo na beti tano hadi kumi linalohimiza utunzaji wa mazingira.

## Miongozo Ya Usahihishaji Ya Kiswahili

Mwongozo ya Usahihishaji kwa Karatasi ya Kwanza

UANDISHI BUNIFU WA KAZA ZA KIFASIHI

**MFANO WA MWONGOZO WA USAHIHISHAJI WA SWALI LA 1, KARATASI YA KWANZA**

**Matokeo Tarajiwa:** Mwanafunzi anatarajiwa kubainisha mbinu za sanaa zilizotumika, kuzichambua na kueleza jinsi zinavyosaidia kuwasilisha ujumbe, akitumia ushahidi kutoka matini.

| Misingi ya tathmini na Viashiria | Alama: 4 | Alama: 3 | Alama: 2 | Alama: 1 |
|---|---|---|---|---|
| 1) **Uelewa wa mbinu za sanaa** *Atambue mbinu za sanaa na kuzifafanua.* | Anatambua mbinu za sanaa 5 na kuendelea na kila mbinu imefafanuliwa kwa usahihi. | Anatambua na kufafanua mbinu za sanaa 3-4 na maelezo ni sahihi. | Anatambua mbinu za sanaa 1-2 na kuzifasili lakini ufafanuzi si kikamilifu. | Anataja mbinu zozote lakini hazifasili ipasavyo. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2) **Ushahidi na uchambuzi wa matini**<br><br>*Ushahidi kutokana na matini na athari za matumizi ya mbinu husika.* | Mbinu 5 na kuendelea zimeambatanishwa na mifano halisi kutoka kwenye matini kwa usahihi na kuonesha sababu ya matumizi ya mbinu husika. | Ameambanisha mbinu 3-4 na mifano sahihi kutokana na matini na amejaribu kufafanua sababu ya matumizi ya mbinu hizo. | -Anaweza kutoa mfano kutokana na makala, lakini ulinganifu wake ni hafifu na amepata changamoto katika ufafanuzi wa sababu za matumizi ya mbinu husika. | Mfano anaoutoa hauhusiani na mbinu iliyotajwa, au hana mfano kabisa au anatoa mifano isiyohusiana na matini. |
| 3) **Umantiki na Matumizi ya Lugha**<br><br>*Umantiki, ufasaha na hitimisho.* | Anaonesha ufahamu wa kina, mantiki, na anatumia lugha fasaha ya kifasihi. | Lugha ni ile inayoeleweka vizuri na uchambuzi unaonesha uelewa wa kutosha | Lugha ni ya kawaida, na kuna dalili za uelewa wa kimsingi. | Uwasilishaji ni dhaifu, na kuna makosa mengi ya lugha na uelewa ni wa juu juu. |

## MFANO WA MWONGOZO WA USAHIHISHAJI WA SWALI LA 2, KARATASI YA KWANZA

**Matokeo Tarajiwa:** Mwanafunzi anatarajiwa kujadili kwa hoja zilizo wazi jinsi haki za wahusika wa kike zinavyoweza kulindwa na kuendelezwa, akitumia mifano mahsusi kutoka katika kazi ya fasihi aliyoisoma na kuonesha uelewa wa mada.

| Misingi ya tathmini na Viashiria | Alama: 4 | Alama: 3 | Alama: 2 | Alama: 1 |
|---|---|---|---|---|
| 1) **Uelewa wa Vipengele vya Dhuluma kwa Wanawake**<br>*Utambuzi wa aina za dhuluma na ufafanuzi wa athari za kijamii na kihisia kwa wahusika wa kike.* | Anatambua na kufafanua zaidi ya aina 5 za dhuluma kwa usahihi, akitaja athari zake kijamii na kihisia kwa kina. | Anatambua na kufafanua aina 3–4 za dhuluma kwa usahihi wa kuridhisha na kueleza baadhi ya athari zake. | Anatambua aina 1–2 za dhuluma, lakini ufafanuzi wake ni wa juu juu au hauna athari ya kijamii. | Hajatambua wala kufafanua ipasavyo aina za dhuluma au amezieleza visivyo. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2) **Ushahidi na uchambuzi wa matini na kupendekeza njia za kupinga dhuluma kwa mwanamke.**<br>*Uwasilishaji wa mifano halisi kutoka katika kazi ya fasihi iliyosomwa na kutoa mapendekezo ya vitendo vya kuhamasisha jamii kukomesha dhuluma kwa wanawake.* | Ametumia mifano 5 au zaidi kutoka matini husika kwa usahihi na amechambua kwa kina jinsi haki za wanawake zinavyolindwa au kudaiwa.<br>Ufafanuzi unaonesha uhusiano wa moja kwa moja na dhamira ya mwandishi.<br>Amefafanua ujumbe wa mwandishi kwa kina na kupendekeza njia 5 au zaidi za vitendo za kuhamasisha jamii kupinga dhuluma dhidi ya wanawake. | Ametumia mifano 3–4 sahihi kutoka matini na kuonesha uelewa wa jinsi haki za wanawake zinavyodhulumiwa na athari zake, ingawa baadhi ya hoja hazijachambuliwa kwa kina. Ameeleza ujumbe kwa usahihi na kupendekeza njia 3–4 za kuhamasisha jamii, ingawa maelezo hayajapanuliwa kikamilifu. | Ametumia mifano 1–2 kutoka matini, lakini uhusiano wake na mada ni hafifu. Uchambuzi ni wa juu juu na hauonyeshi athari za moja kwa moja. Ameeleza ujumbe kwa ujumla bila kutoa mifano thabiti ya njia za uhamasishaji. | Hakuna ushahidi kutoka matini, hoja hazihusiani na kazi ya fasihi; hajaeleza ujumbe wala njia za kuhamasisha jamii, na hata pale ujumbe unapojitokeza, umeelezwa kwa makosa au kwa upungufu mkubwa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3) **Umantiki na Matumizi ya Lugha** *Umantiki, ufasaha na hitimisho.* | Anaonesha ufahamu wa kina, umantiki, na anatumia lugha fasaha ya kifasihi. | Lugha ni ile inayoeleweka vizuri na uchambuzi unaonesha uelewa wa kutosha | Lugha ni ya kawaida, na kuna dalili za uelewa wa kimsingi. | Uwasilishaji ni dhaifu, na kuna makosa mengi ya lugha na uelewa ni wa juu juu. |

**MFANO WA MWONGOZO WA USAHIHISHAJI WA SWALI LA 3, KARATASI YA KWANZA**

**Matokeo Tarajiwa:** Mwanafunzi anatarajiwa kuchanganua kwa hoja zilizo wazi jinsi anavyoweza kuhamasisha jamii kukomesha ukandamizaji wa wanyonge, akitumia mifano mahsusi kutoka katika kazi ya fasihi aliyoisoma na kuonesha uelewa wa mada.

| Misingi ya tathmini na Viashiria | Alama: 4 | Alama: 3 | Alama: 2 | Alama: 1 |
|---|---|---|---|---|
| 1) **Uelewa wa Vipengele vya Ukandamizaji wa Wanyonge**<br>*Utambuzi na ufafanuzi wa aina za ukandamizaji.* | Anatambua na kufafanua zaidi ya aina 5 za ukandamizaji kwa wanyonge kwa usahihi, akieleza athari zake kijamii, kiuchumi na kihisia kwa kina. | Anatambua na kufafanua aina 3–4 za ukandamizaji kwa usahihi na kueleza baadhi ya athari zake. | Anatambua aina 1–2 za ukandamizaji, lakini maelezo ni ya juu juu bila kina cha kijamii. | Anataja aina ya ukandamizaji bila maelezo, anachanganya maana, au hajatambua na kufafanua ipasavyo, hivyo amezieleza visivyo. |
| 2) **Ushahidi na uchambuzi wa matini na njia za kukuza haki za wanyonge** | a) Ametumia mifano mitano au zaidi kwa usahihi kutoka kwenye matini | Ametumia mifano 3–4 sahihi kutoka kwenye matini kuonesha uelewa wa jinsi | Ametumia mifano 1–2, lakini uhusiano wake na mada ni hafifu na uchambuzi ni | Hakuna ushahidi kutoka matini, hoja hazihusiani na kazi ya fasihi; ujumbe haujaelezwa au |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| *Uwasilishaji wa mifano halisi kutoka kazi ya fasihi iliyosomwa na kupendekeza vitendo vya kuhamasisha jamii kukomesha ukandamizaji.* | na amechambua kwa kina jinsi ukandamizaji unavyoonyeshwa na kupingwa.<br>b) Ameeleza kwa kina ujumbe wa mwandishi na kupendekeza njia tano au zaidi za kuhamasisha jamii. | ukandamizaji unavyojitokeza, ingawa hoja hazijachambuliwa kwa kina. Amefafanua ujumbe kwa usahihi na kupendekeza njia 2–3 za kuhamasisha jamii, lakini maelezo hayajapanuliwa vya kutosha. | mdogo. Ujumbe umeelezwa kwa ujumla bila mifano thabiti ya kuhamasisha jamii. | umeelezwa visivyo kwa upungufu mkubwa, na hakuna njia za uhamasishaji zilizooneshwa. |
| 3) **Umantiki na Matumizi ya Lugha** *Umantiki, ufasaha na hitimisho.* | Anaonesha ufahamu wa kina, umantiki, na anatumia lugha fasaha ya kifasihi. | Lugha ni ile inayoeleweka vizuri na uchambuzi unaonesha uelewa wa kutosha | Lugha ni ya kawaida, na kuna dalili za uelewa wa kimsingi. | Uwasilishaji ni dhaifu, na kuna makosa mengi ya lugha na uelewa ni wa juu juu. |

**MFANO WA MWONGOZO WA USAHIHISHAJI WA SWALI LA 4, KARATASI YA KWANZA**

**Matokeo Tarajiwa:** Mwanafunzi anatarajiwa kubainisha na kufafanua uhuru wa kishairi katika shairi husika, akitoa mifano mahsusi kutoka shairi na kuonesha uelewa wa vipengele vya uhuru wa ushairi.

| Misingi ya tathmini na Viashiria | Alama: 4 | Alama: 3 | Alama: 2 | Alama: 1 |
|---|---|---|---|---|
| 1) **Uelewa wa Vipengele vya Uhuru wa Mshairi**<br>*Atambue na kufafanua vipengele vya Uhuru wa Mshairi* | Anatambua na kufafanua vipengele 5 au zaidi vya Uhuru wa Mshairi kwa usahihi. | Anatambua na kufafanua vipengele 3–4 vya ushairi kwa usahihi. | Anatambua vipengele 1–2 lakini ufafanuzi ni wa kijuujuu au si sahihi kikamilifu | Anatambua baadhi ya vipengele bila kuvifafanua, au hawezi kabisa kutambua wala kufafanua vipengele vya uhuru wa mshairi. |
| 2) **Ushahidi na uchambuzi wa shairi.**<br>*Atoe mifano halisi ya vipengele hivyo kutoka kwenye shairi lililotolewa.* | Anatoa mifano halisi 5 au zaidi ya vipengele vya uhuru vya ushairi kutoka katika shairi na anaonesha sababu za | Anatoa mifano 3–4 sahihi ya vipengele vya ushairi kutokana na shairi na kueleza sababu za matumizi yake kwa ufupi. | Anatoa mifano 1–2 ya vipengele vya Uhuru wa Mshairi kutokana na shairi lakini maelezo ya matumizi yake ni hafifu. | Anatoa mifano isiyo sahihi kuhusu vipengele vya uhuru wa ushairi, au hatoi mfano wowote unaoambatana na |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| *Na kufafanua athari za kila kipengele katika kuboresha urari, maana, na mtindo wa shairi.* | matumizi ya kila kipengele kwa mantiki. | | | vipengele vilivyotajwa. |
| 3) **Umantiki, Matumizi ya Lugha na hitimisho**<br>*Mpangilio wa hoja na usahihi wa mawazo na ahitimishe kwa ufasaha wa msamiati wa kifasihi, na matumizi sahihi ya istilahi.* | -Mawazo yamepangwa vizuri kwa mtiririko wa kimantiki, na uchambuzi unaonesha uelewa wa juu.<br>-Lugha ni fasaha, yenye istilahi za kifasihi sahihi, na inadhihirisha ubunifu wa hali ya juu. | -Mawazo yamepangwa vizuri, japokuwa kuna mapengo madogo katika mtiririko.<br>-Lugha ni nzuri, ina makosa machache na istilahi nyingi ni sahihi. | -Kuna mtiririko wa wastani; baadhi ya hoja hazijaunganishwa vizuri.<br>-Lugha ni ya kawaida, ina baadhi ya istilahi sahihi lakini si nyingi. | -Hoja zimechanganyikana na mpangilio ni hafifu.<br>-Lugha ina makosa mengi na istilahi zimechanganywa. |

**Mwongozo ya Usahihishaji kwa Karatasi ya Kwanza**

**UCHAMBUZI WA KAZI ZA FASIHI**

**MFANO WA MWONGOZO WA USAHIHISHAJI KWA SWALI LA KWANZA, KARATASI YA PILI**

**Matokeo Tarajiwa:** Mwanafunzi anatarajiwa kutunga kitendo kimoja cha tamthilia (maneno 1500–2000) akizingatia vipengele vya utunzi na kuonesha suluhisho la suala husika kwa ubunifu.

| Misingi ya tathmini na Viashiria | Alama: 4 | Alama: 3 | Alama: 2 | Alama: 1 |
|---|---|---|---|---|
| 1) **Muundo wa Tamthilia** *Mpangilio wa matukio na uhusiano wa vitendo, maonyesho na wahusika.* | a) Matukio yamepangwa kwa ufasaha (utangulizi, kilele, utatuzi) na yana mtiririko wenye mvuto wa kisanaa.<br>b) Wahusika wanahusishwa vyema katika maendeleo ya hoja kuu. | a) Muundo una mtiririko mzuri, japokuwa baadhi ya sehemu hazijakamilika ipasavyo.<br>b) Wahusika wana mchango unaoeleweka | a) Muundo unaeleweka kwa jumla lakini una mapengo katika mpangilio wa matukio.<br>b) Baadhi ya wahusika hawana uhusiano wa moja kwa moja na hoja kuu. | a) Matukio yamechanganyikana, na muundo hauna utaratibu unaoeleweka. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2) **Vipengele vya Utunzi**<br><br>*Uwasilishaji wa ujumbe husika kupitia Maudhui, wahusika na mandhari* | c) Maudhui makuu yanaibuliwa kwa kina na ujumbe wa kijamii unaelezwa kwa ubunifu.<br>d) -Wahusika ni hai na wanaendana na dhamira, huku mandhari ikionesha uhalisia.<br>e) -Ujumbe wa maadili, uwajibikaji, na suluhisho umeelezwa kwa kina na una mguso wa kijamii. | c) Maudhui yanaeleweka vizuri.<br>d) Wahusika na mandhari vinaendana na ujumbe.<br>e) Ujumbe unaeleweka na unaonesha suluhisho linalowezekana, ingawa halijapanuliwa kikamilifu. | c) -Maudhui yanaeleweka kwa kiasi, lakini hayajachambuliwa kwa kina.<br>d) Wahusika wana sifa chache zilizo wazi.<br>e) Mandhari hayajaelezwa vya kutosha.<br>f) Ujumbe unaonekana lakini haujaelezwa kikamilifu; suluhisho ni la jumla tu. | b) Maudhui hayana msisitizo wa dhamira kuu.<br>c) Wahusika na mandhari havijaendelezwa ipasavyo.<br>d) Ujumbe unaonekana kwa kiwango kidogo na hauna uthabiti. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3) **Matumizi ya Lugha**<br><br>*Matumizi ya mbinu za lugha, ufasaha na umantiki wa kisanaa na hitimisho.* | a) Matumizi ya lugha ni ya kifasihi, yenye mvuto, taswira na tamathali nyingi.<br>b) Lugha ni sanifu, yenye umantiki na ubunifu wa hali ya juu. | Lugha ni fasaha na ina matumizi ya baadhi ya mbinu za kifasihi zinazojenga kazi. | - Lugha ni ya kawaida lakini kuna juhudi za kutumia mbinu za kifasihi. | Lugha ni duni na haina matumizi ya mbinu za kifasihi.<br>- Kuna makosa kadhaa ya kisarufi. |

## MFANO WA MWONGOZO WA USAHIHISHAJI WA SWALI LA 2, KARATASI YA PILI

**Matokeo Tarajiwa:** Mwanafunzi anatarajiwa kutunga shairi la kitarbia lenye beti 5–10, akizingatia vipengele vya utunzi wa ushairi na kuhimiza utunzaji wa mazingira kwa ubunifu.

| Misingi ya tathmini na Viashiria | Mahiri: 4 | Bora: 3 | Wastani: 2 | Msingi: 1 |
|---|---|---|---|---|
| 1) **Uelewa wa Muundo wa Shairi**<br>*Mpangilio wa beti na mishororo* | a) Muundo una ulinganifu kamili wa beti na mishororo.<br>b) Vina na mizani vimezingatiwa kwa ustadi wa kifasihi. | a) Muundo una mtiririko mzuri na vina vimezingatiwa kwa kiasi kikubwa.<br>b) Kuna mapungufu madogo katika mizani. | a) Muundo unaeleweka lakini vina au mizani havijadhibitiwa ipasavyo. | Vina na mizani havina uthabiti; mpangilio wa beti ni wa kubahatisha. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2) **Uwasilishaji wa Maudhui na ujumbe**<br>*Uhusiano wa shairi na mada kuu (utunzaji wa mazingira) na Uwasilishaji wa mafunzo.* | a) Maudhui yameelezwa kwa kina na ubunifu, yakionesha dhamira ya utunzaji wa mazingira kwa ufanisi mkubwa.<br>b) Kila ubeti unaongeza uzito wa ujumbe. | c) Maudhui yanahusu mada kwa uwazi, japokuwa baadhi ya hoja hazijapanuliwa vya kutosha. | b) Mada kuu inaonekana lakini haijashughulikiwa kwa kina; kuna kurudiarudia hoja. | Mada inagusiwa kwa mbali, Maudhui hayana uhusiano na mada, shairi halina msisitizo wa mafunzo ya mazingira. |
| 3) **Matumizi ya Lugha na ufanisi wa kisanaa na hitimisho**<br>*Mbinu za lugha, ufasaha, umantiki, na athari kwa hadhira* | a) Lugha ni ya kishairi.<br>b) Mishororo ina mvuto na umantiki wa kisanaa unaodhihirisha ufasaha.<br>c) Shairi lina ubunifu wa hali ya juu, lina mguso wa kihisia na linahamasisha hadhira. | a) Lugha ni fasaha na inatumia baadhi ya mbinu za kifasihi vizuri.<br>b) Shairi lina ubunifu na linaweza kugusa hisia kwa kiasi. | a) Lugha ni ya kawaida lakini inajitahidi kutumia mbinu za kifasihi.<br>b) Kuna juhudi za ubunifu lakini hazijafanikiwa kikamilifu. | a) Lugha ni dhaifu, haina msisimko wa kisanaa; kuna makosa ya kisarufi.<br>b) Ubunifu ni mdogo; shairi halina mvuto wa kisanaa. |

# 4. MAELEZO YA VIWANGO VYA UTENDAJI.

| Vipengele vinavyohusiana vya Ujenzi wa Uwezo (Construct 1) | KIWANGO CHA UMILISI | UFAFANUZI |
|---|---|---|
| **Uchambuzi na uhakiki wa kazi za fasihi**<br><br>Kuchambua na kuhakiki kazi mbalimbali za nathari, mashairi, tamthilia na riwaya kwa kuzingatia vipengele vya kifasihi ili kuimarisha ustadi wa kuandika, mawasiliano bora, kuelimisha, kuburudisha, kuendeleza na kukuza maadili, pamoja na kujikimu kiuchumi. | Mahiri | Mwanafunzi anaonesha uelewa wa tanzu zote za fasihi. Anachambua na kuhakiki kazi kwa kutumia istilahi sahihi za kifasihi, anatumia mifano halisi kutoka matini teule, na anaweza kuhusisha maudhui na muktadha wa kijamii. Anaonesha ubunifu, uchambuzi wa kiwango cha juu wa mbinu za lugha, dhamira, wahusika, na mitindo. |
| | Bora | Mwanafunzi anaelewa vizuri tanzu za fasihi na anaweza kuchambua kazi kwa usahihi. Anatumia istilahi za kifasihi kwa usahihi na anatoa mifano inayofaa. Anaonesha uelewa mzuri wa maudhui, dhamira, na vipengele vya muundo |
| | Wastani | Mwanafunzi anaelewa baadhi ya vipengele vya fasihi na anaweza kuchambua kazi kwa kiwango cha kuridhisha. Anaweza kutaja baadhi ya mbinu za lugha na dhamira, lakini uchambuzi wake ni wa juu juu au hauna mifano ya kutosha. |

| | | |
|---|---|---|
| | Msingi | Mwanafunzi anaelewa kwa kiasi kidogo. Anaweza kutaja baadhi ya vipengele vya fasihi lakini hawezi kuvieleza kwa kina. Uchambuzi wake hauna muktadha wala mifano ya kutosha. |
| | Msingi Finyu | Mwanafunzi haonyeshi uelewa wa kutosha wa kazi za fasihi. Hajui au anachanganya tanzu za fasihi, na hawezi kufanya uchambuzi wa maana. |
| **Vipengele vinavyohusiana vya Ujenzi wa Uwezo (Construct 2)** | **KIWANGO CHA UMILISI** | **UFAFANUZI** |
| **Utunzi bunifu wa kazi za fasihi**<br><br>Atunge, achapishe na kuandaa kazi bunifu za fasihi kama hadithi fupi, ushairi, nathari, tamthilia na riwaya kwa kuzingatia vipengele vya kifasihi, ili kuburudisha, kukuza maadili, kuimarisha mawasiliano, kujipatia kipato na kuendeleza ustadi wa uandishi bora. | Mahiri | Mwanafunzi anabuni kazi za fasihi zenye ubunifu wa hali ya juu, akitumia mbinu mbalimbali za kifasihi kwa ustadi. Anaonesha uelewa wa mahiri wa miundo ya kifasihi, anatumia lugha ya kuvutia,mtiririko wa mawazo umepangika vizuri na kazi zake zina ujumbe wenye athari kwa msomaji. |
| | Bora | Mwanafunzi anatunga kazi bunilizi kwa ustadi mzuri. Anaonesha matumizi sahihi ya vipengele vya kifasihi kama wahusika, ploti, na mtindo. Kazi ina mtiririko mzuri na ujumbe unaoeleweka. |

| | | |
|---|---|---|
| | Wastani | Mwanafunzi anaweza kutunga kazi bunilizi lakini kwa kiwango cha wastani. Anaonesha ubunifu wa kawaida na matumizi ya baadhi ya vipengele vya kifasihi, lakini kazi yake haijakamilika au haivutii sana. |
| | Msingi | Mwanafunzi anaonesha juhudi za kuandika kazi bunilizi lakini kazi yake haina muundo mzuri, lugha ni duni, na matumizi ya vipengele vya kifasihi ni hafifu au hayapo. |
| | Msingi Finyu | Mwanafunzi hawezi kuandika kazi bunilizi kwa ufanisi. Kazi haina muundo, haieleweki, na haina vipengele vya kifasihi. |




**CONTACT US:**

National Curriculum Development Centre
Plot M838, Kyambogo.
P.O.Box 7002 Kampala, Uganda
+256-393-112-088
**www.ncdc.go.ug**

ISBN 978-9970-494-61-3